FIDIA KWA MANUSURA WA DHULMA ZA KINGONO ZINAZOHUSISHWA NA VURUGU

CHAPISHO LA KENYA

Sajili Maalum ya Manusura wa Dhulma za Kingono Zinazohusishwa na Vurugu (CSRV): Hakuna

Idadi Kamili ya Manusura wa Dhulma za Kingono Zinazohusishwa na Vurugu: 900 (Kulingana na idadi ya watu waliotibiwa katika matawi ya Hospitali ya Nairobi Women's na vituo vingine vya afya ambavyo ni washirika wake wakati wa vurugu za baada ya uchaguzi wa 2007-08. Ushuhuda uliotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali hiyo ulieleza kuwa idadi hiyo ilikuwa "mwanzo mwa mengi yaliyofichika"

Kadirio la Idadi Kamili ya Manusura wa Dhulma za Kingono Zinazohusishwa na Vurugu: Mamia ya Maelefu Wakati wa ukoloni; Zaidi ya 100,000 kati ya mwaka wa 1963-2006; Zaidi ya 10,000 katika uchaguzi wa 2007-8, Chini ya 10,000 kwa uchaguzi wa 2017. Makadirio ya eneo la Magharibi pekee ni zaidi ya wanawake 3000 women na kati ya wanaume 1000-1500.

Mfumo wa Kisheria wa Ndani wa Mpango wa Fidia wa Utawala: Rasimu ya Kanuni ya usimamizi wa fedha za umma (Hazina ya fidia za Dhulma za Kihistoria) iliwasilishwa kwa Idara ya Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuweka katika matumizi fedha zilizo katima hazina hiyo (Ijulikanavyo kama hazina ya Haki ya Urejeshaji au Hazina ya Haki ya bilioni 10), Lakini bado haijakubambitwa na serikali ya Kenya.

Utaratibu wa Kutekeleza Mfumo wa Fidia na Utawala: Hakuna.

Njia za Ndani za Fidia kupitia Mahakama: Ndio, ila kesi chache zimewasilishwa. Zile zilizowasilishwa, zimekwama au kucheleweshwa kwa miaka. Kesi ya kihistoria iliyosababisha uamuzi wa Disemba 10, 2020 (Ombi 122 la mwaka wa 2013 ilichukua zaidi ya miaka saba na sasa ipo kwenye rufaa (Rufaa ya Kiraia Nambari E 645 ya smwaka 2021). Bado hakuna kesi zilizosababisha hatua kamili za ulipaji fidia.

Idadi Tabriban ya Manusura waliopokea aina yoyote maalum ya Fidia ya Dhulma za Kingono Zinazohusishwa na Vurugu: 0.

Mtazamo wa Manusura Kuhusu hali ya Utekelezwaji wa Fidia: Kukata tamaa na kufadhaika baada ya zaidi ya miaka 16 ya ahadi, kupuuzwa, vizuizi, na kutokubali.

Dhulma za Kingono Zinazohusishwa na vurugu Zinazoendelea : Hakuna sasa, ila kulikuwa na hofu na wasiwasi wa kweli kutoka kwa Tume ya Afrika Kuhusu Haki za Binadamu na Watu (ACHPR) kuhusu marudio ya Dhulma za Kingono Zinazohusishwa na Vurugu wakati wa uchaguzi mkuu wa 2022.

Asili na Kiwango cha Dhulma za Kingono zinazohusishwa na Vurugu

Kipindi cha Ukoloni na Mapambano ya Uhuru

Dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu zilikuwa zimeenea Wakati wa ukoloni, zikitumika kwa utaratibu kama njia ya nidhamu, udhalilishaji na kuwapa hofu wanaotaka kuwa wapinzani. Katika harakati za kupigania uhuru, mamia ya maelfu ya wanaume na wanawake walipelekwa kwenye kambi za vizuizi ambako visa vingi ya ubakaji, ubakajiwa makundi, unyanyasaji wa kingono, kuhasiwa, na aina nyinginezo za dhulma za kingono ziliripotiwa.

Vurugu za Kikabila, Kisiasa na Uchaguzi

Dhulma za Kingono ziinazohusishwa na vurugu zimetumika kama zana za kimfumo ili kutisha, kushusha hadhi na kudhibiti jamii zinazochukuliwa kuwa katika upande 'mbaya' wa kisiasa. Maafisa wa ngazi za juu na vikosi vya usalama wameshutumiwa kwa vurugu hizo. Dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu zimejumuisha ubakaji, unajisi, ulawiti, ubakaji wa magenge, ukeketaji (ikiwa ni pamoja na tohara ya kulazimishwa na kukatwa uume). Matukio ya kulazimishwa kutazama au kutekeleza vitendo vya dhulma za kingono dhidi ya wanafamilia yameripotiwa. Manusura na mashahidi pia wameelezea wahalifu kuingiza "bunduki, vijiti, chupa na vifaa vingine kwenye sehemu za siri za wanawake" au kuwapiga sehemu zao za siri kutumia vifaa. Wengi wa walionusurika waliripoti ubakaji wa magenge na kesi nyingi zilizorekodiwa zilihusisha zaidi ya wahalifu wanne na wakati mwingine zaidi ya kumi. Vitendo hivyo vya kikatili pia vimetekelezwa bila hofu ya kuadhibiwa katika miktadha mingine ya vurugu ikiwa ni pamoja na kufurushwa kwa lazima, operesheni za usalama, ukimbizi wa ndani kwa ndani, na katika oparesheni za kukabiliana na ugaidi zinazotekelezwa na maafisa wa serikali ya Kenya. Wanawake na wasichana wanabeba mzigo mkubwa wa Dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu, lakini idadi ya kushangaza ya wanaume na wavulana pia walikuwa manusura wa ukeketaji.

UKWELI NA TAKWIMU

Makadirio ya Utafiti wa GSF

- Mamia ya maelfu ya waathirika wa Dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu katika enzi ya ukoloni
- Zaidi ya Manusura 100,000 katika vurugu kati ya mwaka wa 1963 na 2006
- Zaidi ya Manusura 10,000 katika ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007-8
- Chini ya Manusura 10,000 mwaka wa 2017

"Kubakwa na genge ni jambo moja. Kupata mtoto kutoka ubakaji huo ni jambo jingine.Sikumaliza Shule, nikakataliwa na familia yangu.Nilitaka kujiua pamoja na mtoto wangu…Lakini nimefika umbali huu."

Manusura wa Dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu

Madhara yaliyosababishwa kwa Walionusurika, Familia na Jamii

Athari za Dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu nchini Kenya zimegusa nyanja zote za maisha ya walionusurika. Kwa usaidizi mdogo uliopo, kiwewe kwa wanawake, wanaume na watoto waliozaliwa kutokana na ubakaji kimesababisha changamoto zinazoendelea za afya ya akili, hali ya kiafya na ulemavu uliokithiri. Walionusurika huzungumza kuhusu kunaswa, kutoweza kuepuka visa hivyo vya zamani na kulaumiwa na kuepukwa kwa kile kilichotokea, mara nyingi wakikabiliwa na unyanyasaji wa maneno na/au kimwili. Wengi waliachwa na waume zao baada ya kubakwa na wameachwa na aibu na maumivu yasiyofutika mioyoni mwao. Watoto waliozaliwa kutokana na ubakaji huongeza zaidi kiwewe na makovu, na kuwaongezea aibu. Waume, familia au wanajamii hutumia maneno ya uchungu kuwashusha hadhi kwa shutuma: "lazima uliwajua wahaliokudhulumu; ni kosa lako."

Kutotambuliwa kisheria,wahalifu Kutekeleza vitendo hivyo bila ya hofu ya kuadhibiwa na fidia huchangia uchungu wa walionusurika huku **unyanyapaa na lawama** ukibadilisha kwa kiasi kikubwa mwelekeo wao wa maisha, kuathiri ustawi wao wa akili, afya ya kimwili, hali ya kijamii na kiuchumi. Kwa watoto waliozaliwa kutokana na ubakaji, athari ni unyanyasaji usiolezeka na kutengwa na mama zao, wanafamilia na Jamii kwa ujumla. Wengi wanakabiliwa na matatizo ya kihisia na kisaikolojia. Watoto walioshuhudia Dhulma za kingono dhidi ya wazazi wao pia wameingiwa na kiwewe kwa kujua kwamba wazazi wao ni manusura na wanaepukwa na jamii.

Kila changamoto mpya ya maisha ni ukumbusho mkali wa siku za nyuma. Manusura walidhibitsha hili kwa njia tofauti:

"Nilikuwa nikifanya kazi na nilikuwa na mshahara, biashara yangu imeharibiwa, vitu vya nyumbani vimeharibiwa, shule ya watoto kuharibiwa, ndoa -imevunjika."

"Nimefanywa kuwa ombaomba bila heshima."

"Kabla ya vurugu kuzuka, tulikuwa tukiishi maisha mazuri. Tulikuwa na biashara zetu, tulikuwa na kazi na watoto wetu walikuwa wakienda shule. Tungeweka pesa hata kwenye benki, tulikuwa tunakula na kuvaa vizuri. Watoto wetu waliwajua baba zao. Kulikuwa na upendo, amani na heshima katika familia na jamii zetu. Kufanya maamuzi ilikuwa rahisi

kwa sababu tulikuwa na pesa. Sasa hali hizi zote zimebadilika kabisa kuwa kinyume."

"Nilikuwa meneja wa kiwanda huko Nakuru na nilikuwa na gari langu, lakini vurugu hizo zimenirudisha nyuma"

Kenya ni jamii ya mfumo dume ambako kanuni za kidini na kijamii na kitamaduni huleta ukosefu wa usawa na ule wa jinsia. Kushindwa kuchunguza ipasavyo na kushtaki uhalifu mkubwa kumesababisha utamaduni wa wakosaji Kutokuwa na hofu ya kuadhibiwa. Wahalifu wametiwa moyo na ukosefu wa uwajibikaji, kama ilivyodhihirishwa na kuenea zaidi kwa dhulma za kingono zilizoripotiwa katika uchaguzi wa 2017, ambao haujakuwa na dalili za kurekebisha hali hadi tarehe 28 Oktoba 2022, wakati Noordin Haji, Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma alipotoa taarifa kupitia vyombo vya habari -akikiriiri kwamba kweli kuna ushahidi wa kuunga mkono mashtaka ya ubakaji "kukiwa na uwezekano wa kupatikana na hatia " chini ya sheria ya kimataifa ya uhalifu, Na. 16 ya 2008. Mkurugenzi wa mashtaka ya umma ametoa maagizo kwamba washukiwa washtakiwe ipasavyo.

Mitazamo ya Walionusurika

Mahitaji na Matarajio

Walionusurika wanadai fidia inayohusiana na **"uwepo wetu wenyewe, maisha yetu na ya watoto wetu**". Walionusurika wanaamini kuwa fidia ni haki yao, kimaumbile na kwa sababu serikali ilijitolea kuwaunga mkono. Wengi walionusurika hutumia maneno kulipwa na fidia kwa kubadilishana, kumaanisha matarajio ya msaada wa kifedha wa Serikali. Miaka 16 baada ya ghasia za baada ya uchaguzi wa 2007-8, mazungumzo kuhusu ulipaji fidia yanasalia kuwa mchakato wa kuwanyima haki. Kwa wale ambao haki zao zilikiukwa, fidia inachukuliwa kuwa muhimu kuanza upya na kuwafanya wakamilifu: fidia inachukuliwa kuwa mwisho wa Kipindi hicho cha mateso.

Juhudi za kusaidia uhuru wa kiuchumi zinahitajika ili kukabiliana na umaskini na ongezeko la waathirika kuwa kwenye hatari kutokana na yale yaliyotokea.

Betty Okero kutoka vuguvugu la CSO Network anaeleza*: "Baadhi yao wanaishi sokoni kwa sababu hawana pa kwenda. Watoto wao wanarudishwa nyumbani kwa kukosa karo, hata ndugu na jamaa wanaojiweza hawawezi kusaidia. manusura wameathirika kisaikolojia, kama vile watoto wao ambao wana matatizo ya afya ya akili pia. Baadhi ya watoto wanakua na kuwa watu wenye uchungu sana na jeuri. Walishuhudia. Wanahitaji msaada wa kisaikolojia.*"

Onyesho la maeneo ambako kesi za Dhulma za Kingono zinazohusishwa na uchaguzi zilirekodiwa wakati wa uchaguzi wa Kenya wa 2017. Kulingana na: Tume ya Kitaifa ya Haki za Binadamu ya Kenya (KNCHR)

Juhudi za Manusura

Mbinu Maalum Kuwasilisha Kesi Mahakamani: Mnamo 2013, manusura wanane wa Dhulma za Kingono wakati wa vurugu za 2007-8 waliwasilisha Ombi (Na. 122 la 2013) katika Mahakama Kuu. Katika uamuzi wa kihistoria wa tarehe 10 Desemba 2020, Kitengo cha katiba na haki za kibinadamu cha Mahakama Kuu, kilitambua dhulma za kingono za 2007-8 kwa mara ya kwanza na kushindwa kwa serikali kuchunguza na kushtaki ukiukaji uliotendeka. Mahakama iliwatunuku manusura wanne milioni nne kila mmoja (takriban Dola 35,000 za marekani). Hata hivyo, uamuzi huo haukutambua wajibu wa Serikali na kushindwa kuwalinda raia dhidi ya Dhulma za Kingono zinazohusiana na vurugu hata wakati kesi haziripotiwi kwa polisi. Waliowasilisha Ombi hilo wamekataa rufaa kwa baadhi ya uamuzi wa mahakama kuu kwa misingi kuwa kuna mianya katika uamuzi wa haki ya fidia. Kesi zingine kutoka maeneo mengine nchini zimewasilishwa lakini zimegubikwa na ucheleweshaji na vizuizi. Hazina ya Fidia kwa dhulma za Kihistoria ilipaswa kugharamia malipo rasmi, lakini bila kanuni zilizo wazi za kusimamia hazina hiyo, Manusura wa Dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu hawajanufaika.

Maombi Kwa Bunge: Mnamo mwaka wa 2015, wahusika kutoka asasi za kiraia wakiwemo walionusurika waliandaa kampeni na kuliomba bunge kujadili ripoti ya Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano (TJRC) iliyotolewa mwaka 2013. Ripoti hiyo ilichapishwa kwa sehemu tu (sehemu za dhulma za kingono na Ukiukaji mwingine wa Haki za Kibinadamu hazikuzingatiwa) na haikujadiliwa na Bunge la Kitaifa mwaka 2015. Takriban miaka 10 imepita tangu ripoti ya TJRC iwasilishwe, lakini mjadala na kupitishwa kwake bado havijatendeka katika Bunge la Kitaifa.

Kubuniwa kwa Mfumo wa "Hazina ya Fidia kwa Dhulma za Kihistoria": Mnamo 2015, Tume ya Kitaifa ya Haki za Kibinadamu ya Kenya (KNCHR) iliongoza mashauriano ya kisekta mbalimbali ili kutekeleza " Hazina ya fidia za Dhulma za Kihistoria" iliyotangazwa na Rais Kenyatta mwaka wa 2015. Wahusika kutoka mashirika ya kiraia walijumuisha wanachama wa vuguvugu la haki ya mpito (TJN) vuguvugu la kitaifa la Manusura na waathirika (NVSN), Tume ya Kurekebisha Sheria ya Kenya (KLRC) pamoja na Ofisi ya Kamishna Mkuu wa Umoja wa Mataifa wa Haki za Kibinadamu. Mnamo 2017, hati mbili ziliwasilishwa kwa Idara ya Haki na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali:

- Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma (Hazina ya fidia za Dhulma za Kihistoria) Kanuni za 2017, ambazo zimeambatanishwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma; na
- Sera ya Hazina ya fidia za Dhulma za Kihistoria.

Ombi kwa Seneti : Mnamo 2019, vuguvugu la kitaifa la Manusura na Waathirika (NVSN) iliwasilisha ombi katika bunge la Seneti, ikitaka miongoni mwa maombi mengine, kwamba Seneti izingatie na kupitisha Ripoti ya TJRC ambayo Bunge la Kitaifa lilishindwa kuzingatia. Baadaye, Jacqueline Mutere, kutoka Grace Agenda na Wachira Waheire, kutoka NVSN

walialikwa kuzungumza mbele ya Kamati ya Kudumu ya Haki, Masuala ya Kisheria na Haki za Kibinadamu. Mnamo 2020, Kamati hiyo ilipendekeza masuala hayo yawasilishwe ili yajadiliwe katika Seneti, lakini hayakujadiliwa kamwe.

Hafla ya Manusura Kuzungumza: Mnamo Juni 2021, katika Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu, wahusika kutoka mashirika ya kiraia Jaqueline Mutare, Mwanzilishi wa Grace Agenda na Betty Abade-Okero, Mkurugenzi wa vuguvugu la CSO Network (Kisumu), pamoja na vuguvugu la haki ya mpito (TJN) na NVSN , kwa usaidizi kutoka Global Survivors Fund, waliandaa hafla ya kipekee ya "Manusura Kuzungumza" ili kuwashirikisha viongozi wa Serikali. Hafla hiyo ilipeperushwa moja kwa moja kwa mtandao na kuchochea mchango kutoka watumizi wa mitandao katika kampeni iliyofikia zaidi ya watu milioni 2.8 kupitia hashtegi #SurvivorsSpeakKE na #ActForReparations.

Fidia

KWA NADHARIA

Ahadi za Kisiasa

- Mnamo Oktoba 2008, Tume ya Waki (Tume ya Uchunguzi kuhusu dhulma za Kingono Baada ya Uchaguzi) ilitambua rasmi dhulma za Kingono zilizotekelezwa baada ya uchaguzi wa 2007-8, ikihusisha wajibu mkubwa wa polisi.
- Mnamo 2015, Rais Uhuru Kenyatta aliomba Msamaha kwa Umma "makosa ya zamani" na kuahidi bilioni 10 za Kenya kwa " Urejesho wa haki" . Tarehe 4 Aprili 2019, Rais Kenyatta alithibitisha kujitolea kwake kubuni hazina ya shilingi 10 bilioni za Kenya ili "kuponya majeraha ya malalamiko ya kihistoria ambayo kwa muda mrefu yameathiriwa na siasa zetu na uhusiano mbaya wa kijamii", lakini hakuna hatua zilizopigwa kuhusu swali hili tangu wakati huo.
- Mnamo 2020, katika Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa, serikali ilijitolea ku:
    - kukubali ukiukaji dhidi ya Manusura wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu
    - Kutekeleza fidia kwa Manusura wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu
    - Kuimarisha Juhudi za kupata suluhu ya vurugu za baada ya uchaguzi wa 2007 na 2017

Suluhu za Mahakama

- Mnamo Desemba 2008, Rais Kibaki na Waziri Mkuu Odinga walikubali kuanzisha jopo Maalum na Kutekeleza kikamilifu mapendekezo ya Tume ya Waki.
- Mnamo 2012, Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) ilianzisha kesi dhidi ya wahalifu wa Ngazi ya Juu wa vurugu za baada ya uchaguzi wa 2007-8
- Mnamo tarehe 10 Disemba 2020, Mahakama Kuu ya Kenya kihistoria iliwatambua Manusura wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu kuanzia 2007-8, na kuwapa fidia waathirika wanne wa dhulma hizo.

Suluhu za Kiutawala

- Mwaka 2013, Serikali ilichapisha (ilitangaza) Ripoti ya TJRC, ambayo ilipendekeza fidia.
- Mwaka 2017, rasimu ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma (Hazina ya fidia ya dhulma za Kihistoria) ziliandaliwa ili matumizi ya fedha katika hazina hiyo yaanze .
- Mnamo Machi 2021, Serikali iliripoti kwa Kamati ya Haki za Kibinadamu ya Umoja wa Mataifa kwamba Bodi ya Kulinda Waathiriwa ilikuwa imeanza majukumu yake

KWA VITENDO

Ahadi za Kisiasa

- Serikali ya Kenya haijawahi kuwatambua au kuwakubali waathiriwa wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu kutoka 2007-8 au vurugu za baada uchaguzi wa 2017, au kukubali kuhusika kwa polisi katika vurugu hizo.
- Ombi la msamaha kwa umma la 2015 la rais Uhuru lilitambua dhulma zingine za baada ya uchaguzi lakini sio dhulma za Kingono zilizojiri
- Wahalifu wametiwa moyo na tamaduni ya kutoadhibiwa, iliyothibitishwa na kuenea kwa dhulma za Kingono wakati wa vurugu za uchaguzi wa 2017
- Polisi walipongezwa na Rais kwa ulinzi wao wakati wa uchaguzi wa 2017 kama "kazi iliyofanywa vizuri." Asilimia 54.6 ya waathiriwa katika utafiti wa KNCHR waliwatambua Polisi kama wahalifu wa vitendo hivyo.

Suluhu za Mahakama

- Bunge la Kenya lilipiga kura na kukataa mswada wa kubuni jopo maalum la kuwasikiliza waliohusika, jambo lililosababisha Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu (ICC) kuanza uchunguzi kwa hiari yake mwaka wa 2010.
- Mnamo 2013, watu wa Ngazi ya Juu walioshtakiwa na ICC walichaguliwa kuwa Rais na Naibu Rais wa Kenya. Kufikia 2016, kesi za ICC zilisambaratika kutokana na vitisho vya mashahidi na kutoshirikiana.
- Ingawa uamuzi wa Mahakama Kuu ya 2020 ni uamuzi wa kihistoria katika mambo mengi, fidia ilitolewa kwa walalamishi wanne tu kati ya wanane walionusurika na kuwasilisha kesi mahamakani. Kesi hiyo bado inaendelea katika Mahakama ya Rufaa kufikia Januari 2023, huku zaidi ya miaka 10 ikiwa imepita.

Suluhu za Kiutawala

- Ripoti ya TJRC ya mwaka 2013 iliyochapishwa kwenye Gazeti la Serikali iliacha sehemu IIA na IIC, ambazo zilitoa maelezo kuhusu dhulma za kingono na unyanyasaji mwingine uliojiri
- Hazina ya Haki ya Urejesho ilipokea awamu yake ya kwanza ya shilingi bilioni 3.4 za Kenya (takriban dola millioni 30.9 za marekani) katika mwaka wa kifedha wa 2016-2017, Lakini Hakuna rekodi ya jinsi fedha hizo zilitumika kutokana na ukosefu wa kanuni.
- Rasimu ya mfumo wa kisheria wa 2017 wa kuanza matumizi ya hazina ya fidia kwa dhulma za Kihistoria haijawahi kupitishwa.
- Huduma za Bodi ya Ulinzi wa Waathiriwa (fidia, urekebishaji, malipo na ulinzi maalum) haziangazii waathiriwa wa dhulma za kihistoria (yaani vurugu za baada ya uchaguzi wa 2007-8). Fidia itatolewa tu na Bodi baada ya kupokea amri ya mahakama

Fursa

Ingawa kuna ukosefu wa tumaini miongoni mwa Manusura na kuchoka miongoni mwa wanaharakati, kuna fursa za kuendelea na mchakato huu. Hazina ya dhulma za Kihistoria imetangazwa, na katika kiwango cha kiufundi hatua zinazohitajika ili ianze kufanya kazi ni chache. Kuna mifano ya ulipaji fidia, ikijumuisha malipo kwa wakimbizi wa ndani kwa ndani mwaka 2007-8, hata kama si ya uwazi au thabiti katika maeneo yote. Uamuzi wa kihistoria wa Mahakama Kuu ya 2020, huku rufaa yake ikiendelea, unakubali madhara yaliyosababishwa kwa walionusurika na kuthibitisha haki ya walionusurika ya kulipwa fidia na mapungufu ya serikali. Inatoa fursa zaidi ya kutaka megeuzi, kama vile ahadi za serikali ya Kenya zilizotolewa katika Baraza la Haki za Kibinadamu la Umoja wa Mataifa la 2020 (ona Katika Nadharia hapo juu).

Katika hali ya kuangazia matakwa ya Manusura yaliyoibuka kwenye Kikao chao mnamo Juni 2021, kumekuwa na ahadi za kutia moyo kutoka kwa washirika wapya watatu wa Serikali, akiwemo Mbunge Mhe. Esther M Passaris; Leah Nyambeki ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Ulinzi wa Waathiriwa na Mhe. Daktari Linah Jebii Kilimo ambaye ni Katibu Mkuu katika Wizara ya Utumishi wa Umma na Jinsia.

Vuguvugu dhabiti la walionusurika, likiungwa mkono na kujitolea kwa mashirika ya kiraia na washirika wengine, ikiwa ni pamoja na washirika wa kimataifa, ni muhimu kwa mafanikio. Vuguvugu hizi na ushirikiano tayari upo, na kwa pamoja zina uwezo mkubwa. Pamoja na hayo, mipango, kampeni na miito ya kutaka mageuzi inayoendeshwa kwa mpango itahitaji kudumishwa kwa wakati. Wanaharakati wengi wamepoteza matumaini na kuendelea na kazi zao zingine. Fursa za kuweka masuala hai na kupiga hatua zinahitaji hasa:

- Kudumisha kasi na motisha waliyopata Manusura kupitia Utafiti wa Kimataifa wa Fidia wa shirika la GSF, kuwawezesha walionusurika kushirikisha umma kwa ujumla, kubuni kikundi cha wasaidizi na kuzungumza na viongozi wao;
- Kufuatilia ahadi zilizotolewa na maafisa na viongozi wa kisiasa wakati wa Kikao cha "Manusura Kuzungumza" kilichoandaliwa tarehe 22 Juni 2021;
- Kuangazia katika siku za mbeleni wito uliotolewa wakati wa kampeni ya siku 16 za kushinikiza mageuzi iliyokamilika tarehe 16 Desemba 2022;
- Kufuatilia kuendelea kwa shughuli za Bodi ya Kulinda waathiriwa katika kuhakikisha utekelezaji mzuri wa sheria ya kulinda Waathiriwa Sheria Na. 17 ya 2014;
- Kudumisha kasi ya ombi la Kikatiba la 122 ya 2013 ambalo sasa lipo kwenye rufaa kama Rufaa ya Kiraiya nambari E 645 ya 2021 (Kumbumbuku ya pili ya uamuzi huo ilikuwa tarehe 10 Desemba 2022), na kuendeleza kwa mpango harakati za kupata Suluhu mahakamani.
- Kusaidia na kuupa umarufu Mradi wa Ukumbusho unaotolewa na vuguvugu la kitaifa la waathiriwa na Manusura, kuhakikisha kwamba unaonyesha ukubwa wa athari za dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu; na
- Kukuza kasi na kuwapa motisha Manusura ili wazungumze na viongozi wa maeneo yao, hasa viongozi wa ngazi ya Kaunti kwa mfano huko Kisumu ambapo uhusiano kati ya mawakili wa mashirika ya kijamii na viongozi tayari umeanzishwa.

Changamoto Kuu

- **Ukosefu wa nia ya kisiasa:** Baada ya miaka 15 ya kukwepa kuangazia swala hili, Manusura wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu bado wanangoja fidia. Serikali zilizofuata zimetambua tu waathiriwa kama wale watu waliouawa na kuhamishwa makwao kutokana na vurugu, bila kuwatambua walionusurika na dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu au waathiriwa wengine. Majaribio ya kuwazuia Manusura wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu wanaodai fidia kwa kuwaaibisha , vitisho na kuwaogopesha pia yameripotiwa.
- **Uchovu wa walionusurika na kutokuwa na tumaini:** Kulingana na shuhuda za walionusurika, kuhusika kwao na dhulma za kingono imekuwa jambo la kusikitisha, na licha ya juhudi za miaka 15, fidia bado ni ngumu. Kudumisha kasi na kuhakikisha hatua zinapigwa ni jambo la msingi katika hali hii ya uchovu na kukosa matumaini.
- **Ukosefu wa msaada kwa watoto waliozaliwa kutokana na ubakaji, ambao sasa wana umri wa miaka 15:** Athari mbaya za kisaikolojia, kijamii na kiuchumi kwa mamia ya watoto waliozaliwa kutokana na ubakaji zinaendelea bila kutambulika, huku watoto kutoka 2007-8 sasa ni vijana waliobalehe na waliopoteza fursa na wana makovu makuu.
- **Ukosefu wa takwimu kamili:** Idadi ya jumla ya Manusura inayonukuliwa ni sehemu ndogo ya zile zinazohesabiwa na wataalam walioko nyanjani. Pale wataalam wamefanya tathmini katika baadhi ya maeneo, takwimu zimekuwa kubwa zaidi kuliko ilivyoripotiwa, hasa kwa wanaume walionusurika. "*Ikiwa tungekuwa na utafiti unaozingatia idadi, sote tunapaswa kushtushwa na matokeo*", anasema Betty Abade-Okero, Mkurugenzi, vuguvugu la CSO Network linalofanya kazi katika

Maeneo ya Magharibi.

- **Utamaduni wa sasa wa kutokuwa na hofu ya kuadhibiwa , hulka ya wanasiasa ya kutobadili misimamo au kutokubaliana kuhusu jambo fulani na kutekwa nyara kwa asasi za serikali na viongozi wenye nia binafsi:** Ubinafsishaji wa afisi ya rais na kulemaza kwa makusudi taasisi za umma, ambao umekua chini ya kila Rais tangu uhuru ni changamoto kubwa. Inasisitiza "*dhana iliyoenea kwamba urais huleta manufaa kwa kabila la Rais*", ambayo, kwa sehemu, inaelezea motisha za jamii kutekeleza vurugu ili kupata au kulinda mamlaka bila kujali matokeo ya matendo yao au kujali raia wenzao.

Mapendekezo

Kwa Serikali ya Kenya

Uwajibikaji

- Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Idara ya Haki inapaswa kushughulikia visa ya kutenda vitendo bila hofu ya kutoadhibiwa kwa kuchunguza na kushtaki uhalifu wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu uliotekelezwa mwaka wa 2007-8 na 2017.
- Rais anapaswa kutambua rasmi na kutambua mahususi hali ya walionusurika na dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu na madhara makuu waliyopata.
- Serikali inapaswa kuchukua hatua mara moja kuchapisha ripoti kamili ya TJRC, ikijumuisha sehemu IIA na IIC, ikifuatiwa na mjadala wa bunge unaojumuisha mazungumzo ya dhulma za kingono na aina nyingine za vurugu; na kutekeleza mapendekezo yake ya fidia kwa waathiriwa wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu.
- Idara za serikali zinafaa kushirikiana na Hazina ya Kimataifa ya Mahakama ya Jinai katika mpango wa kuwasaidia waathiriwa na kutumia mafunzo kutoka kwa mradi huo kuanzisha mpango wa fidia wa kitaifa unaongozwa na serikali.
- Tekeleza hatua za kiishara kama vile ukumbusho, suluhu za kielimu na kitamaduni, na mageuzi ya kisheria na kitaasisi ili kuhakikisha kutojirudia kwa makosa katika mchakato unaoongozwa na walionusurika.
- Wizara ya Utumishi wa Umma, Jinsia na usawa lazima iunde jopo, litakalojumuisha wahusika wakuu katika nafasi hii, wakiwemo walionusurika kuwaelekeza washirika katika serikali kuwezesha haki ya fidia kuwa kweli.

Hazina ya Haki ya Urejesho

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali na Idara ya Haki inapaswa kupitisha rasimu ya Kanuni za Usimamizi wa Fedha za Umma (Hazina ya Fidia kwa dhulma za kihistoria) Kanuni za 2017 na Sera, ili kuweka katika matumizi Hazina ya Haki ya Urejesho

Hii ni pamoja na:

- Kutuza fidia za jumla zinazowaangazia Manusura na haswa kwa Manusura wa dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu , ikijumuisha fidia ya kifedha, au hatua nyinginezo kama zilivyopendekezwa na walionusurika, kama vile hatua za urekebishaji, elimu, kuwawezesha kimaisha ,usaidizi wa kimatibabu na kisaikolojia.
- Kuweka hatua madhubuti za kuwapa watoto waliozaliwa kwa kubakwa msaada wa kisaikolojia, kupata elimu, na hatua nyinginezo ili kushughulikia ipasavyo matokeo ya ukiukwaji huo na unyanyapaa na kukataliwa ambao wamekabiliana nao.
- Mchakato ulio salama na huru, ulio na wafanyikazi waliofunzwa vya kutosha, kusajili kwa njia salama aina mbalimbali za waathiriwa, ikiwa ni pamoja na walionusurika na dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu, kutambua athari za vurugu na mahitaji yao ya fidia. Mchakato huo unapaswa kuhakikisha usaidizi wa kisaikolojia kwa waathirika ili waweze kujitokeza. Hii inapaswa kupitia shirika linaloaminika ili kutoa fidia kwa uwazi kwa walionusurika.
- Ufadhili upatikane kupitia bajeti za kitaifa na kuwekwa katika mipango ya miaka ijayo.
- Mpango wa ulipaji fidia unapaswa kuwaweka kipaumbele Manusura wenye ulemavu, na pia kutambua athari za dhulma kwa vizazi, ili kujumuisha msaada kwa ya familia ya Manusura baada ya kifo chao.
- Ili kuhakikisha kuridhika na kutorudiwa kwa makosa, Serikali inapaswa kufadhili ipasavyo na kuanza kutekeleza sera ya mwaka 2014 ya kuzuia na kushugulikia visa vya dhulma za kijinsia, kuwapa usalama, usaidizi wa kisaikolojia, usaidizi wa kijamii na kiuchumi, msaada wa kisheria na rufaa kwa waathiriwa na Manusura wa dhulma za kingono

Kwa Taasisi za Serikali

- Mahakama inapaswa kuharakisha mchakato wa kusikilizwa na kuamuliwa kwa kesi ya rufaa iliyowasilishwa na raiya Na. E 645 ya 2021 (Ikikataa rufaa kwa hukumu ya Mahakama Kuu katika Ombi la Kikatiba Na. 122 la 2013), ili kuthibitisha wajibu wa serikali wa kuzuia na kushugulikia ipasavyo dhulma za Kingono zinazohusishwa na vurugu ikiwa ni pamoja na kutoa Suluhu za kudumu na fidia kwa waliothariwa.
- Mamlaka Huru ya kutathmini utendakazi wa polisi inapaswa kuangazia hulka ya vitendo vya polisi na vikosi vya usalama Kutekeleza majukumu yake bila hofu ya kuadhibiwa na Serikali inapaswa kuhakikisha marekebisho ya kimfumo ya vyombo vyote vya kutekeleza sheria.

Mapendekezo (imeendelea)

Kwa asasi za Kiraia

- Kusaidia mipango inayoongozwa na walionusurika au inayowaweka kipaumbele Manusura kwa ajili ya kuboresha maisha yao, ikijumuisha kupitia shughuli za uponyaji wa kiwewe, na msaada kufanikisha kujitegemea kiuchumi. Mipango inayoongozwa na wanawake imethibitishwa kuunda maeneo salama kwa wanaume, yakiwaruhusu Kuzungumzia yanayowakumba.
- Kuimarisha mipango inayoongozwa na walionusurika au inayowaweka kipaumbele Manusura ili kuendeleza, kuratibu na kukuza kampeni za kushurutisha mageuzi zinazolenga watekelezaji wajibu katika ngazi za kaunti na kitaifa.
- Kusaidia mashirika ya kaunti na ya kitaifa ya walionusurika, pamoja na vuguvugu za walionusurika ili kushiriki katika kubadilishana maarifa, mshikamano, na usaidizi kati ya kaunti
- Kushirikiana na washirika wa kitaifa na mabingwa ambao wanaweza kufanya kazi kama mabalozi ili kukusanya umati muhimu wa wasemaji wanaotetea utekelezaji wa hatua za fidia.
- Kufanya kazi na watendaji wa kimataifa na wafadhili kama vile Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa, Mataifa rafiki na shirika la Global Survivors Fund katika kuuliza maswali kuhusu ukosefu wa hatua kupigwa na usaidizi wa kiufundi au mwingine unaohitajika katika kuwezesha utekelezaji wa programu ya fidia inayoongozwa na Serikali.

"Nataka fidia Ili maisha yangu yawe Kama yalivyokuwa hapo awali."

Manusura wa dhulma za Kingono Zinazohusishwa na vurugu

Hatua zifuatazo

Hatua za haraka za jumuiya ya kimataifa, mashirika ya kiraia ya Kenya, na mamlaka za Serikali zinahitajika ili kusaidia, kuunga mkono na kudumisha juhudi za walionusurika ili kuafikia mapendekezo yaliyo hapo juu na kupata kutambuliwa na fidia ifaayo.

Kufuatia uchaguzi wa amani mnamo Agosti 2022, Serikali hii ina fursa ya kuonyesha dhamira ya Kenya kwa ajenda ya haki za binadamu na jinsi inavyotimiza wajibu chini ya sheria kwa manusura wa vurugu za uchaguzi mnamo 2007/2008 na 2017. Kwa kuongoza ajenda ya uponyaji, serikali inaweza kutekeleza wajibu huu kwa walionusurika kama watekelezaji wa wajibu kwa kundi hili. Katika kipindi cha miaka 15 iliyopita, walionusurika wameandaa kampeni za michakato ya fidia ili kuboresha maisha yao na yale ya wanao, kwa kushughulikia fursa zilizopotea kama vile elimu na kurekebisha mahusiano ya kijamii.

Ajenda ya ulipaji fidia inapatikana ndani ya ajenda ya Serikali ya Kenya ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, huku idadi kubwa ya walionusurika wakiwa wanawake. Hata hivyo ni muhimu pia kushughulikia dhulma dhidi ya wanaume na wavulana, pamoja na kushughulikia haki na mahitaji ya watoto waliozaliwa kutokana na kubakwa. Kutoa Suluhu la suala hili kutaupa umaarufu uwezo wa Manusura kuendelea na maisha Mbali na makosa ya zamani

Kenya ina njia nyingi za kuwaokoa walionusurika, sasa ni wakati wa kutekeleza hili kwa vitendo.

GLOBAL SURVIVORS FUND
FOR AND WITH SURVIVORS OF CONFLICT-RELATED SEXUAL VIOLENCE

Grace-Agenda
Grace for full recovery

Civil Society Organisation Network
ONE VOICE ONE PURPOSE